SHERIA YA MAMLAKA YA UDHIBITI WA USAFIRI ARDHINI
(SURA 413)
Imetengenezwa chini ya Kanuni ya 45(2(i))

# KANUNI ZA KUFIFILISHA MAKOSA ZA MAMLAKA YA UDHIBITI USAFIRI ARDHINI ZA MWAKA 2023

MPANGILIO WA KANUNI

*Kanuni* *Jina*

SEHEMU YA KWANZA
VIFUNGU VYA AWALI

1. Jina
2. Matumizi
3. Tafsiri

SEHEMU YA PILI
HATUA ZA KUFIFILISHA MAKOSA

4. Taarifa ya makosa
5. Utaratibu baada ya notisi ya makosa
6. Utaratibu baada ya kukataa kosa
7. Malipo ya faini
8. Utekelezaji wa amri ya kufifilisha kosa

SEHEMU YA TATU
VIFUNGU VYA JUMLA

9. Hatua za Mamlaka
10. Taarifa kwa Mkurugenzi wa Mashitaka

MAJEDWALI

Tangazo la Serikali Na. ……………… la tarehe …………………

SHERIA YA MAMLAKA YA UDHIBITI WA USAFIRI ARDHINI
(SURA 413)

# KANUNI

(Zimetengenezwa chini ya Kanuni ya 45(2(i))

## KANUNI ZA MAMLAKA YA UDHIBITI USAFIRI ARDHINI ZA UFIFILISHAJI WA MAKOSA ZA MWAKA 2023

## SEHEMU YA KWANZA
## MASHARTI VYA AWALI

Jina

1. Kanuni hizi zitajulikana kama Kanuni za Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini za Ufifilishaji wa Makosa za Mwaka 2023

Matumizi

2. Kanuni hizi zitatumika kufifilisha makosa kama yalivyoainishwa chini ya Sheria na Sheria za kisekta.

Tafsiri

3. Katika Kanuni hizi isipokuwa kama itakapoelezwa vinginevyo-

Sura 413

"Sheria" maana yake ni Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini;

"Mamlaka" maana yake ni Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini iliyoanzishwa chini ya kifungu cha 4 cha Sheria;

Sura 413

"Mkurugenzi Mkuu" maana yake ni Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka aliyeteuliwa kwa mujibu wa kifungu cha 15 cha Sheria;

## SEHEMU YA PILI
## HATUA ZA KUFIFILISHA MAKOSA

Taarifa ya makosa

4. (1) Pale ambapo mtu ametenda kosa kinyume cha Sheria au sheria za kisekta, Mamlaka itamjulisha kosa lake kwa kujaza fomu ya kufifilisha makosa kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Kwanza la Kanuni hizi.

(2) taarifa iliyoainishwa kwenye kanuni ndogo ya (1) ita-

(a) ainisha kosa lililotendwa na kifungu kilichokiukwa;
(b) ainisha adhabu mahsusi kwa makosa yaliyotendwa na kiasi cha ufifilishwaji; na
(c) onesha tarehe na sahihi ya Afisa wa Mamlaka.

Utaratibu baada ya notisi ya makosa

5. (1) Mtu atakayepokea notisi chini ya kanuni ya 4(1) atatakiwa kukubali au kuonesha nia ya kujibu tuhuma dhidi ya kosa.

(2) Endapo mtu atakiri kosa kwa mujibu wa Kanuni ndogo (1), atatakiwa kujaza fomu ya kukiri kosa kama ilivyoainishwa kwenye Jedwali la Pili la Kanuni hizi na Mamlaka itafifilisha kosa hilo.

(3) Endapo mtu ataonesha nia ya kujibu mashtaka dhidi ya kosa, atatakiwa kujaza Fomu ya nia ya kujibu mashtaka, kama ilivyoainishwa kwenye Jedwali la Tatu la Kanuni hizi.

(4) Mtu atakayeshindwa au kukataa kusaini Fomu ya Notisi ya makosa atachukuliwa kuwa amepinga kutenda kosa, na Mamlaka itaendelea na utaratibu ulioanishwa katika kanuni ya 6.

Utaratibu baada ya kupinga kutenda kosa

6. Endapo mtu ataonesha nia ya kujibu mashtaka dhidi ya kosa, Mamlaka itawasilisha Fomu ya Notisi ya makosa pamoja na Fomu ya Nia ya Kujibu Mashtaka kwa Mkurugenzi wa Mashtaka pamoja na taarifa nyingine yoyote inayohusika kwa hatua zaidi.

Malipo ya faini

7. (1) Mtu atakayekiri kutenda kosa kwa mujibu wa kanuni ya 5(2), atatakiwa kulipa kwa Mamlaka kiasi cha fedha ambacho ni nusu ya faini ambayo angetozwa endapo angepatikana na hatia.

(2) Endapo mtu atashindwa kulipa kiasi cha fedha kilichofifilishwa katika kipindi cha siku 14 kuanzia tarehe ya kukiri kosa iliyoainishwa katika Fomu ya kukiri kosa, Mamlaka itatoza riba ya asilimia tano kwa mwezi ya kiasi ambacho hakijalipwa.

(3) Endapo kiasi kilichofifilishwa pamoja na riba hakitalipwa kwa zaidi ya siku tisini kuanzia tarehe ya kutolewa kwa taarifa ya notisi ya makosa, Mamlaka itatoa Notisi ya ukiukaji kama ilivyoainishwa kwenye Jedwali la Nne la Kanuni hizi.

Utekelezaji wa amri ya kufifilisha kosa

8. Mamlaka inaweza kuwasilisha Amri ya kufifilisha kosa kwenye Mahakama yenye Mamlaka ya kukazia Amri hiyo kwa ajili ya utekelezaji.

## SEHEMU YA TATU
## MASHARTI YA JUMLA

Hatua za Mamlaka

9. Amri ya ufifilishaji wa makosa haitaathiri hatua za Mamlaka zinazoweza kuchukuliwa kwa ajili ya kulinda athari zinazoweza kuwapata watu, mali au kulinda masuala yanayohusu maslahi ya umma.

Taarifa kwa Mkurugenzi wa Mashtaka

10. Mamlaka itawasilisha taarifa ya makosa yaliyofifilishwa kwa kila robo ya mwaka kwa Mkurugenzi wa Mashitaka ikibainisha:

(a) jina na taarifa za aliyetenda kosa;
(b) kosa na kifungu cha sheria husika kilichokiukwa;
(c) tarehe na sehemu kosa lilipotendeka;
(d) kiasi kilichofifilishwa pamoja na riba kama ipo; na
(e) taarifa nyingine yoyote ile kadri Mkurugenzi wa Mashitaka anaweza kuzihitaji.

# MAJEDWALI

## JEDWALI LA KWANZA

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

SHERIA YA MAMLAKA YA UDHIBITI WA USAFIRI ARDHINI

(SURA 413)

FOMU YA NOTISI YA MAKOSA

*(Chini ya Kanuni ya 4(1))*

Kwa .......................................................................... wa anuani ......................................................

1. Unashitakiwa kwa makosa yafuatayo:

   (a) ................................................ kinyume na........………………… ya ….........................................

   (b) ................................................ kinyume na ........…………………ya ….........................................

   (c) ................................................ kinyume na ........………………... ya ….........................................

2. ENDAPO unakiri kutenda makosa tajwa hapo juu unatakiwa kujaza "FOMU YA KUKIRI KOSA" iliyoambatishwa na utawajibika kulipa kiasi kilichofifilishwa kama ifuatavyo:

| Na. | Kosa | Faini iliyoainishwa kwa mujibu wa Sheria | Kiasi kilichofifilishwa |
|---|---|---|---|
| | | | |
| | | | |
| | | | |

3. ENDAPO unapinga kutenda kosa unatakiwa kujaza "FOMU YA NIA YA KUJIBU MASHTAKA" iliyoambatishwa, pamoja na majibu yako na kuwasilisha kwa Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ndani ya siku 7 kuanzia tarehe ya kupokea fomu hii.

....................................................
Mkurugenzi Mkuu/Afisa aliyeidhinishwa

……………………………………
Saini

Tarehe: .........................................

Saini: ……………………………

Imepokelewa na: ……………………

Tarehe: ………………………….

JEDWALI LA PILI

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

SHERIA YA MAMLAKA YA UDHIBITI WA USAFIRI ARDHINI

(SURA 413)

FOMU YA KUKIRI KOSA

*(Chini ya Kanuni ya 5(2))*

Mimi .......................................... wa ...................... (anuani) nikiwa (mmiliki/mkurugenzi/meneja/mwakilishi) wa ............................................................................... (kampuni/ushirika n.k) nakiri kutenda kosa/makosa ………………………………… Kama yalivyoainishwa kwenye Fomu ya Notisi ya makosa.

Ninaomba Mamlaka ififilishe makosa tajwa kwa mujibu wa Kifungu/Kanuni …………………………….. ya ………………………………………………………….. Sheria/Kanuni.

Nathibitisha kuwa nitalipa kiasi kilichofifilishwa cha Shilingi ………………………………………. ndani ya muda wa siku kumi na nne kutokana na makosa yaliyoorodheshwa katika Fomu ya Notisi ya makosa.

Ninafahamu kwamba riba ya asilimia tano kwa mwezi itatozwa iwapo kiasi cha fedha kilichofifilishwa hakitalipwa ndani ya muda ulioainishwa hapo juu

Saini: ................................................................................... Tarehe: .......................................................

Utambulisho …………………………………………………(NIDA/LESENI YA UDEREVA N.K.)

Saini ya alinayepokea fomu ya kukiri kosa ……………………………………….

Saini ya Afisa Aliyeidhinishwa.......................................................................

## JEDWALI LA TATU

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

SHERIA YA MAMLAKA YA UDHIBITI WA USAFIRI ARDHINI

(SURA 413)

**FOMU YA NIA YA KUJIBU MASHITAKA**

*(Chini ya Kanuni ya 5(3))*

Mimi .......................................... wa ..................... ( anuani) nikiwa (mmiliki/mkurugenzi/meneja/mwakilishi) wa ......................................................................... (kampuni/ushirika) nakusudia kujibu mashtaka kama yalivyoainishwa kwenye Fomu ya Notisi ya makosa.

Natoa maelezo yangu kwa maandishi kukana makosa tajwa kama ilivyoambatishwa pamoja na fomu hii.

Saini: ............................................... Tarehe: ......................................................

Utambulisho ………………………………………………(NIDA/LESENI YA UDEREVA N.K.)

JEDWALI LA NNE

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

SHERIA YA MAMLAKA YA UDHIBITI WA USAFIRI ARDHINI

(SURA 413)

**NOTISI YA UKIUKAJI**

*(Chini ya Kanuni ya 7(3))*

Kwa ...................................................................... wa ………………………………………… (anuani)

UNATAARIFIWA KWAMBA umeshindwa kulipa kiasi kilichofifilishwa cha Shilingi …………………………….. kilichotakiwa kulipwa kama ilivyoainisha katika Fomu ya Kukiri kosa iliyoambatishwa na fomu hii.

UNATAARIFIWA KWAMBA kwa kukiuka kwako kulipa kiasi kilichofifilishwa kama ilivyoelezwa hapo juu kimesababisha Mamlaka kutoza kiasi cha riba ya asilimia 5 ya kiasi ambacho hakijalipwa kwa mwezi cha Shilingi ……………………………………….. na hivyo kuwa Shilingi ……………………. kwa mwezi.

UNATAARIFIWA ZAIDI KWAMBA endapo utashindwa kulipa kiasi kilichofifilishwa pamoja na riba ndani ya muda wa siku saba (7) kuanzia tarehe ya kupokea notisi hii, kutailazimu Mamlaka kuwasilisha suala hili kwenye Mahakama yenye uwezo kwa ajili ya kukazia utekelezaji dhidi yako.

Mkurugenzi Mkuu/Afisa aliyeidhinishwa

Saini: ……………………………   Tarehe: …………………………….

Imepokelewa na: ………………………………………… Saini: ………………… Tarehe : ………………

Imetolewa na:

Dodoma,   Makame Mbarawa,
………....,  2023   *Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi*